# HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI NA VYAMA VYA SIASA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA MWL. J. K. NYERERE TAREHE 01 AGOSTI, 2020

- **Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Sera, Bunge na Uratibu),**
- **Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Wanahabari,**
- **Mabibi na Mabwana.**
- **Habari za Asubuhi!**

Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine siku ya leo kwa ajili ya kikao hiki muhimu. Kikao hiki ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu hasa tunapoelekea katika Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020. Aidha, niwashukuru kwa kuitikia wito wetu wa kuhudhuria kikao hiki ambacho kinalenga kutoa taarifa ya maandalizi na maelekezo mbalimbali kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, lakini pia ni katika kutimiza ahadi yetu ambayo tumekuwa tukiitoa kwenu mara kwa mara ya kuwashirikisha katika hatua mbalimbali za michakato ya uchaguzi kwa kadri inavyowezekana. **Karibuni sana**.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Vyama vya Siasa ni wadau Wakuu na muhimu wa Uchaguzi Mkuu kwani ndio wahusika wakuu wa moja kwa moja katika mchakato wa uchaguzi. Kutokana na ukweli huo, Tume imeona umuhimu wa kufanya kikao cha pamoja ili kupeana taarifa na kufahamishana kuhusu maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Vilevile, kikao hiki ni nafasi ya kubadilishana na kupeana uzoefu wa utekelezaji wa shughuli za uchaguzi ili kuhakikisha tunaepusha dosari ambazo zinaweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Katika maandalizi, Tume imekamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao ulifanyika mara mbili kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Awamu ya kwanza ilianza tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020 kwa nchi nzima na uboreshaji wa awamu ya pili ulifanyika kuanzia tarehe 17 Aprili, 2020 na kukamilika tarehe 04 Mei, 2020.

Awamu ya pili ya uboreshaji ilifanyika sambamba na uwekaji wazi wa Daftari la awali kwa awamu ya kwanza katika vituo 37,814 vilivyotumika katika zoezi la uboreshaji awamu ya kwanza. Tume iliendesha zoezi la uwekaji wazi wa Daftari la awali kwa awamu ya pili kwa siku 4 kuanzia tarehe 17 - 20 Juni, 2020 ambapo Daftari lilibandikwa katika vituo vyote vilivyotumika wakati wa uandikishaji awamu ya kwanza.

Katika awamu zote mbili za uboreshaji, jumla ya Wapiga Kura wapya **7,326,552** waliandikishwa sawa na asilimia **31.63** ya Wapiga Kura **23,161,440** walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, Jumla ya Wapiga Kura **3,548,846** waliboresha taarifa zao na Wapiga Kura **30,487** waliondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria. Baada ya kutoa

Wapiga Kura ambao taarifa zao zimejirudia, Daftari kwa hivi sasa lina jumla ya Wapiga Kura wapatao milioni **29,188,347.**

Kutokana na idadi hiyo ya wapiga kura, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kutakuwa na vituo **80,155 vya** kupigia kura na kila kituo kimoja kitakuwa na Wapiga Kura wasiozidi 500.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hakukuwa na marekebisho katika Sheria za Uchaguzi. Hata hivyo, Tume imefanya maboresho ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Vile vile imekamilisha Maelekezo ya Uchaguzi kwa ajili ya wadau mbalimbali na Watendaji wa Uchaguzi.

Aidha, Tume ilishirikiana nanyi kuandaa Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020. Sheria, Kanuni, Maadili na Vitabu hivyo vya maelekezo mtapatiwa baada ya kikao hiki. Hivyo, naomba mzisome na kuzielewa nyaraka hizo ili ushiriki wenu uwe na ulete tija katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Ili kuwa na uwazi katika zoezi la Uchaguzi Mkuu, Tume imekuwa ikiwashirikisha wadau wa uchaguzi, mukiwemo ninyi, katika hatua

mbalimbali za mchakato wa Uchaguzi. Mathalan, kabla ya kuanza zoezi la uboreshaji, Tume ilifanya maboresho ya Kanuni, ambapo ilikutana na Vyama vya Siasa na kupokea maoni yao. Pia, kabla ya kuanza zoezi la uboreshaji wa majaribio uliofanyika kati ya tarehe 29 Machi, 2019 na 4 Aprili, 2019 Tume ilivitaarifu Vyama vya Siasa kuhusu zoezi hilo na kupokea maoni yao kuhusu namna bora ya kulitekeleza, ambapo Vyama vilipata nafasi ya kuweka Mawakala wakati wa zoezi la uboreshaji.

Maeneo mengine ya ushirikishwaji wa wadau yalihusu nyaraka zinazohusu zoezi la uboreshaji ambapo Tume ilivipatia Vyama vya Siasa orodha ya vituo vya uandikishaji vya nchi nzima, Kanuni za Uboreshaji na ratiba ya zoezi zima la uboreshaji, ili kuviwezesha kujipanga katika ushiriki wa zoezi la uboreshaji kikamilifu. Vilevile, Tume kwa mamlaka iliyonayo chini ya kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ilitoa vibali kwa Asasi za Kiraia Kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Aidha, Tume imekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali ikiwemo Vyama vya Siasa, Vyombo vya Habari, Viongozi wa Dini na Makundi Maalum kama vile Wanawake, Vijana, Watu Wenye Ulemavu, Asasi za Kiraia na katika maeneo mengine Wazee wa Kimila. Mikutano hii ilifanyika pia katika kila

mkoa kabla ya kuanza zoezi la uandikishaji wa wapiga kura katika mkoa husika.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kama ambavyo imeripotiwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, Tume ya Taifa ya Uchaguzi tayari imetoa ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kama ambavyo mmesikia, Uchaguzi Mkuu umepangwa kufanyika siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020 na tayari serikali imetoa tamko kupitia Gazeti la Serikali Na. 578 la tarehe 24 Julai 2020 ambapo siku hiyo itakuwa ni siku ya mapumziko.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Fomu za Uteuzi zitaanza kutolewa tarehe 5 Agosti, 2020 kwenye Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jijini Dodoma kwa wagombea wa Kiti cha Rais. Fomu kwa ajili ya Ubunge na Udiwani zitatolewa kwenye Makao Makuu ya Halmashauri yalipo Majimbo na Kata husika kuanzia tarehe 12 hadi 25 Agosti, 2020.

Aidha, urejeshaji wa fomu utafanyika tarehe 25 Agosti, 2020 kabla ya saa 10 kamili jioni ambayo ndiyo siku ya uteuzi. Naomba kutoa rai kwenu kuzingatia ratiba hiyo na kuwasisitiza wagombea kutoka katika vyama vyenu kujaza fomu kwa usahihi ili kuepuka dosari zinazoweza kuwafanya kushindwa kuteuliwa.

Katika kipindi cha Uteuzi, Wagombea pia wanahaki ya kisheria ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea mwenzake. Aidha, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya Siasa nao ni miongoni mwa waliopewa haki ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea yoyote.

Uzoefu unaonyesha kuwepo kwa malalamiko yanayotolewa katika kipindi cha Uteuzi bila kuwasilishwa kwenye mamlaka sahihi za kisheria na bila kufuata hatua stahiki ikiwemo hii ya kuweka pingamizi. Katika hatua hii, muweka pingamizi na aliyewekewa pingamizi wanahaki ya kukata Rufaa kwenye mamlaka husika pale ambapo hawataridhika na maamuzi ya wasimamizi wa uchaguzi.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi, kipindi cha kampeni za uchaguzi kitaanza tarehe 26 Agosti, 2020 hadi tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kuzingatia ratiba ya uchaguzi iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) Kampeni za uchaguzi kwa upande wa Tanzania Zanzibar zitaishia tarehe 26 Oktoba 2020 ili kupisha upigaji wa kura ya mapema ya Rais wa Zanzibar, Mwakilishi na Diwani. Hivyo mpange ratiba zenu za kampeni ambazo zitaishia tarehe 26 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Katika kipindi cha kampeni, vyama vyenu vitapata fursa ya kuwanadi wagombea nakuelezea sera na Ilani za

Uchaguzi za vyama vyenu. Katika eneo hili, uzoefu unaonyesha kuwa kipindi cha Kampeni kunakuwa na joto kali la kisiasa linatokana na baadhi ya watu kukosa uvumilivu wa kisiasa hali ambayo inaweza kuhatarisha amani na utulivu wa nchi. Napenda kutoa rai kwenu na wafuasi wenu na kuwasihi kufanya kampeni za kistaarabu na hivyo kuepuka kufanya vitendo vitakavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani na utulivu wa Nchi yetu.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kama mnavyokumbuka, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishirikiana nanyi pamoja na Serikali katika kuandaa Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ambayo yalisainiwa na pande zote mnamo tarehe 27 Mei, 2020. Ni matumani yangu kuwa mtasoma na kuelewa ipasavyo Maadili haya, ambayo mbali na Sheria nyingine za Nchi; yanasimamia michakato ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na mienendo ya Kampeni za Uchaguzi na yameweka makatazo mbalimbali kwa kubainisha mambo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kufanywa na Tume, Serikali na Vyama vya Siasa.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Maadili ya Uchaguzi, pamoja na mambo mengine, yanavitaka Vyama vya Siasa kufanya Kampeni za kistaarabu na kuepuka kufanya fujo au kuchochea vurugu ya aina yoyote katika mikutano

ya vyama vingine; kutokutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu, rangi au maumbile kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni; viongozi wa vyama vya siasa, wagombea na wafuasi wao kutokubeba silaha yoyote ikiwa ni pamoja na silaha za jadi au zana yoyote inayoweza kumdhuru mtu katika mikutano na shughuli zote za Kampeni au mkusanyiko wowote wa kisiasa.

Nawasihi kusoma na kuzingatia ipasavyo Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ili kuepuka usumbufu unaoweza kuwapata na kuathiri haki yenu ya kufanya Kampeni kwa ajili ya kunadi wagombea wenu na kuelezea sera zenu.

Pamoja na kuelezea na kunadi Sera na Ilani za uchaguzi za vyama vyenu, kipindi cha Kampeni kitumike pia kuwahamasisha wananchi hasa Wapiga Kura waliojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kujitokeza kwa wingi siku ya Kupiga Kura.

Aidha, Maadili hayo yanahusisha pia mamlaka ya uundaji wa Kamati za Maadili kuanzia Ngazi ya Kata, Jimbo, Taifa na Rufaa. Nawashauri tuzitumie kamati hizi kipindi cha Kampeni pale kunapokuwa na malalamiko kwani, zimepewa uwezo wa kisheria wa kushughulikia malalamiko kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa

na wajumbe wake ni pamoja na wawakilishi wa vyama vitakavyoshiriki uchaguzi katika ngazi husika.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kumekuwepo na malalamiko kwa baadhi ya Watendaji wa Uchaguzi kutokuwepo ofisini wakati wa Uteuzi wa wagombea. Kitendo cha aina hii ni kinyume na Maadili ya Uchaguzi na kwa namna yoyote hakikubaliki. Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zinawataka Watendaji wa Uchaguzi kuwa katika maeneo yao ya kazi muda wote wakati wa kipindi cha Uteuzi wa Wagombea, Upigaji Kura na katika hatua yoyote ya mchakato wa Uchaguzi.

Tume tayari imekutana na Wasimamizi wote wa Uchaguzi kwa upande wa Tanzania Bara tarehe 24 Julai, 2020 Jijini na Dodoma ambapo msisitizo ulitolewa kwa wao kuzingatia Maadili ya Uchaguzi na maelekezo yanayotolewa na Tume. Aidha, Wasimamizi wa Uchaguzi tayari wamekwisha kuteuliwa na wanaendelea na mafunzo ambayo yatakamilika tarehe 03 Agosti 2020.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 58 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292 na kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, Mawakala wa Vyama vya Siasa wataruhusiwa kuwepo

katika Vituo vya Kupigia Kura. Jambo hili ni la muhimu kwani linasaidia kudhihirisha uwazi katika zoezi zima. Wajibu wa Mawakala wa Vyama vya Siasa ni kuangalia kama Sheria, Kanuni, na Taratibu zilizowekwa na Tume zinazingatiwa katika mchakato mzima wa kupiga Kura na kutangaza matokeo. Pia, kulinda maslahi ya vyama na wagombea wao katika vituo vya kupigia na Kuhesabia Kura na maeneo ya kujumlishia Kura.

Tume katika maelekezo yake imeainisha utaratibu utakaotumika katika kuwatambulisha mawakala hawa wakati wa uchaguzi. Nawasihi kuzingatia taratibu za kuwatambulisha mawakala wenu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanazingatia takwa la kisheria la kula kiapo cha kutunza siri kwa wakati. Aidha, muwasisitize kuzingatia masharti ya kisheria katika kutekeleza jukumu la uwakala.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Nitumie nafasi hii pia kuwafahamisha maeneo mengine muhimu katika kufanikisha Uchaguzi Mkuu kama vile bajeti na vifaa vya uchaguzi. Tume iliandaa Bajeti ya kiasi cha **Tsh. 331,728,258,035.00** zinazotarajiwa kutumika katika kuandaa na kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Kwa kuzingatia kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, itagharimia shughuli zote za Uchaguzi kwa asilimia mia moja.

Katika eneo la vifaa vya uchaguzi Tume inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali sambamba na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo. Jumla ya zabuni ishirini na tano (25) zimetangazwa ambazo zinahusisha Uchapishaji wa nyaraka mbalimbali za uchaguzi, ununuzi wa vituturi, masanduku ya kura, vifaa vya Elimu ya Mpiga Kura na uchapishaji wa karatasi za kura. Baadhi ya vifaa vimekwisha kamilika na vimeanza kupokelewa katika Bohari ya Tume.

Eneo lingine muhimu katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu ni Elimu ya Mpiga Kura, kama tunavyofahamu kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 kinaipa mamlaka Tume ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima kuratibu na kusimamia Taasisi au Asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Tume kwa upande wake imejipanga kutoa elimu hiyo kwa njia mbalimbali ikiwemo Vyombo vya Habari, Mitandao ya Kijamii, Machapisho mbalimbali, Mikutano na wadau kupitia wawakilishi wao, kushiriki katika maonesho na matamasha mbalimbali pia kutumia gari la Matangazo la Tume kwa ajili ya kukutana na wananchi ana kwa ana.

Tume pia ilialika Asasi za Kiraia na Taasisi kwa ajili ya kuomba kupata vibali vya kutoa Elimu ya Mpiga Kura wakati wa Uchaguzi Mkuu. Baada ya uhakiki, jumla ya asasi 252 zilikidhi vigezo na hivyo kupatiwa vibali. Kati ya Asasi hizo, saba (7) ni kutoka Tanzania Zanzibar.

Tume inatarajia kukutana na Asasi hizo mikoani ili kuwapitisha katika Mwongozo wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura wanaopaswa kuutumia na kuufuata katika kipindi chote cha zoezi hili.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Katika ushirikishaji wa wadau, Tume pia ilialika Watazamaji wa Uchaguzi wa ndani ambapo ilitoa mwaliko kwa Asasi na Taasisi za ndani zenye nia ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi kuleta maombi. Baada ya mchakato wa uhakiki, jumla ya Asasi 97 zilizokidhi vigezo tayari zimepewa taarifa na zinasubiri kupewa vibali wakati ukifika.

Kwa upande wa Watazamaji wa Uchaguzi wa Kimataifa mwaliko umetolewa na zoezi la kupokea maombi linaendelea. Wakati ukifika tutawajulisha idadi ya waombaji hao.

Pia nichukue fursa hii kuwafahamisha kuwa, katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Tume haikuchunguza na kugawa Majimbo ya Uchaguzi. Ilibadilisha majina ya Majimbo ya **Chilonwa** kuwa **Chamwino** na **Mtera** kuwa **Mvumi**. Majimbo hayo yote yapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeridhia mipaka ya majimbo kama ilivyorekebishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilibadilisha jina la Jimbo la Kijitoupele na kuliita Pangawe, na Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeridhia matumizi ya jina hilo. Kama ilivyokuwa katika uchaguzi wa 2015, Idadi ya majimbo ya uchaguzi imebaki 264, ambapo Tanzania Bara ina Majimbo 214 na Tanzania Zanzibar ina Majimbo 50. Idadi ya Kata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu itakuwa ni 3,956.

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Tume ina matumaini makubwa ya kufanikisha Uchaguzi huu kwa kutegemea ushiriki wenu katika hatua zote zilizosalia kufikia siku ya uchaguzi, imani hii inatokana na ushirikiano mlioonesha wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Mmekuwa wepesi wa kuwasilisha hoja na ushauri na kutaka ufafanuzi pale inapohitajika kila tunapokutana nanyi katika vikao mbalimbali.

Kwa mara nyingine, napenda kuwashukuru tena kwa kuitikia wito na kushiriki kikao hiki muhimu kwetu sote. Tume itaendelea

kuwashirikisha kwa kadri itakavyowezekana na kama kawaida itasimamia uchaguzi huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni naTaratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi. Lengo ikiwa ni kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 unakuwa huru, wa uwazi, wa haki na wa kuaminika kwa kuweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki.

Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka rasmi kuwa kikao chetu kimefunguliwa rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**